JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUHUSU UAMUZI WA RUFAA DHIDI YA UAMUZI WA WASIMAMIZI WA UCHAGUZI KWA PINGAMIZI ZA UTEUZI WA WAGOMBEA UBUNGE KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO NA UDIWANI KWA TANZANIA BARA**

**Dodoma, Tarehe 03 Septemba, 2025**

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 53 na 65 vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 vikisomwa pamoja na kanuni ya 29(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea jumla ya rufaa hamsini na moja (51) za kupinga uamuzi wa wasimamizi wa uchaguzi kuhusu pingamizi za Uteuzi wa wagombea Ubunge katika Jamhuri ya Muungano na Udiwani kwa Tanzania Bara.

Kati ya rufaa hamsini na moja (51) zilizopokelewa na kufanyiwa uamuzi, rufaa ishirini (20) ni za kupinga uamuzi wa wasimamizi wa uchaguzi kuhusu Ubunge na rufaa thelathini na moja (31) ni kupinga uamuzi kuhusu Udiwani.

Aidha, rufaa kumi na tatu (13) kati ya rufaa hamsini na moja (51) zilitolewa uamuzi katika kikao cha Tume cha tarehe 31 Agosti, 2025 na taarifa yake ilitolewa kwa Umma tarehe hiyo.

Tume katika kikao chake kilichofanyika kuanzia tarehe 01 hadi 03 Septemba, 2025, imefanya uamuzi wa rufaa thelathini na nane (38), ambapo kwa rufaa za Ubunge, Tume imezikubali rufaa nne (04), imekataa rufaa saba (07) na kufuta

rufaa moja (01). Kwa upande wa rufaa za Udiwani, Tume imekubali rufaa tisa (09) na kuzikataa rufaa kumi na saba (17), kama inavyoainishwa kwenye mchanganuo ufuatao:-

**1.0. Rufaa za ubunge zilizokubaliwa:**

Zifuatazo ni rufaa nne (04) za wagombea ubunge zilizokubaliwa: -

i. **Ndugu Mvungi Lucas Felix** mgombea ubunge Jimbo la Mwanga kupitia Chama cha NCCR-Mageuzi dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Mwanga;

ii. **Ndugu Anaeli Roiya Nasari** mgombea ubunge Jimbo la Arumeru Mashariki kupitia Chama cha ACT-Wazalendo dhidi ya **Ndugu Joshua Samwel Nassari** wa Chama cha Mapinduzi;

iii. **Ndugu Ngwada Mubarak Twaha** mgombea ubunge Jimbo la Mafinga Mjini kupitia Chama cha CHAUMMA dhidi ya **Ndugu Villa Lutevele Nathan Dickson** kupitia Chama cha Mapinduzi; na

iv. **Ndugu Matiko Esther Nicholas** mgombea ubunge Jimbo la Tarime Mjini kupitia Chama cha Mapinduzi dhidi ya **Ndugu Kangoye Jackson Ryoba** mgombea ubunge kupitia Chama cha ACT-Wazalendo.

Hivyo, kwa wagombea kuanzia namba ***i*** ya kirumi hadi namba ***iii*** ya kirumi, Tume imetengua uamuzi wa wasimamizi wa uchaguzi na kukubali rufaa za wagombea hao. Wagombea tajwa waendelee na taratibu za kampeni za ubunge katika majimbo wanayogombea.

Kuhusu mrufaniwa katika namba ***iv*** ya kirumi ambaye ni **Ndugu Kangoye Jackson Ryoba**, Tume imetengua uteuzi wake na kumuondoa katika orodha ya wagombea ubunge Jimbo la Tarime Mjini.

## 2.0. Rufaa za ubunge zilizokataliwa:

Zifuatazo ni rufaa saba (07) za wagombea ubunge zilizokataliwa:-

i. **Ndugu Gimbi Dotto Masaba** mgombea ubunge Jimbo la Itilima kupitia Chama cha CHAUMMA dhidi ya **Ndugu Njalu Daudi Silanga** kupitia Chama cha Mapinduzi Jimbo la Itilima;

ii. **Ndugu Omary Ahmad Badwel** mgombea ubunge Jimbo la Bahi kupitia Chama cha CHAUMMA dhidi ya **Ndugu Keneth Ernest Nollo** mgombea ubunge kupitia Chama cha Mapinduzi jimbo la Bahi;

iii. **Ndugu Mohamed Juma Haji** mgombea ubunge Jimbo la Chambani kupitia Chama cha AAFP dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi jimbo la Chambani;

iv. **Ndugu Loyce Benjamin Giboma** mgombea ubunge Jimbo la Ubungo kupitia Chama cha CHAUMMA dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Ubungo;

v. **Ndugu Pius Ismail Masuruli** mgombea ubunge Jimbo la Bunda Mjini kupitia chama cha ACT-Wazalendo dhidi ya **Ndugu Esther Ernest Bulaya** mgombea ubunge kupitia Chama cha Mapinduzi jimbo la Bunda Mjini;

vi. **Ndugu Kangoye Jackson Ryoba** mgombea ubunge Jimbo la Tarime Mjini kupitia Chama cha ACT-Wazalendo dhidi ya **Ndugu Matiko Esther Nicholas** mgombea ubunge kupitia Chama cha Mapinduzi Jimbo la Tarime Mjini; na

vii. **Ndugu Salum Khamis Salum** mgombea ubunge Jimbo la Meatu kupitia Chama cha Mapinduzi dhidi ya **Ndugu Rosemary Kasimbi Kirigini** mgombea ubunge kupitia Chama cha ACT-Wazalendo Jimbo la Meatu.

Kwa wagombea kuanzia namba *i* ya kirumi hadi namba *iv* ya kirumi, Tume imekubaliana na uamuzi wa wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo husika wa kutowateua kugombea nafasi ya ubunge katika majimbo husika.

Aidha, kwa warufaniwa namba *v* ya kirumi hadi namba *vii* ya kirumi ambao ni **Ndugu Esther Ernest Bulaya** wa Jimbo la Bunda Mjini, **Ndugu Matiko Esther Nicholas** wa Jimbo la Tarime Mjini na **Ndugu Rosemary Kasimbi Kirigini** wa Jimbo la Meatu, Tume imekubaliana na uamuzi wa wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo husika kuhusu uteuzi wao, hivyo, waendelee na taratibu za kampeni za Ubunge.

**3.0. Rufaa ya Ubunge iliyofutwa**

Tume imefuta rufaa ya ubunge iliyowasilishwa na **Ndugu Flatei Gregory Massay,** mgombea ubunge Jimbo la Mbulu Vijijini kupitia Chama cha ACT-Wazalendo kwa kuwa imepitwa na matukio (*overtaken by events*) baada ya mrufani kujitoa kugombea kwa mujibu wa kifungu cha 70(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 kikisomwa pamoja na kanuni ya 32(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025.

**4.0. Rufaa za udiwani zilizokubaliwa:**

Zifuatazo ni rufaa tisa (09) za wagombea udiwani zilizokubaliwa: -

i. **Ndugu Abdurahamani Mohamedi Matulano** mgombea udiwani Kata ya Mijelejele, Jimbo la Lulindi kupitia Chama cha ACT-Wazalendo dhidi **Ngugu Juma Ramadhani Polle** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi kata ya Mijelejele, Jimbo la Lulindi;

ii. **Ndugu Anafi Salumu Nandala** mgombea udiwani Kata ya Ndomoni, Jimbo la Nachingwea kupitia Chama cha ACT-Wazalendo dhidi ya **Ndugu Raymondi Erasto Vitusi** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Ndomoni, Jimbo la Nachingwea;

iii. **Ndugu Charles Bakari Hokororo** mgombea udiwani Kata ya Namwanga, Jimbo la Lulindi kupitia Chama cha ACT-Wazalendo dhidi ya **Ndugu Yusuph Bushiri Mlaponi** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Namwanga, Jimbo la Lulindi;

iv. **Ndugu Lulu Omari Bakari** mgombea udiwani Kata ya Rahaleo, Jimbo la Lindi Mjini kupitia chama cha NCCR- Mageuzi dhidi ya **Ndugu John Stephen Mmuni** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Rahaleo, Jimbo la Lindi Mjini;

v. **Ndugu Mackrina Chales Nyoni** mgombea udiwani Kata ya Mkongo, Jimbo la Namtumbo kupitia Chama cha ACT-Wazalendo dhidi ya **Ndugu Daniel Magnus Nyambo** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Mkongo, Jimbo la Namtumbo;

vi. Ndugu **Mabula Ng'welemi Bugali** mgombea udiwani Kata ya Sagata, Jimbo la Itilima kupitia Chama cha CUF dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Itilima;

vii. **Ndugu Richard Africa Mwangomale** mgombea udiwani Kata ya Lufilyo, Jimbo la Busokelo kupitia Chama cha CHAUMMA dhidi ya **Ndugu Emanuel Seth Mwakajegela** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Lufilyo, Jimbo la Busokelo;

viii. **Ndugu William Daniel Baliyakula** mgombea udiwani Kata ya Buseresere, Jimbo la Chato Kusini kupitia Chama cha ACT-Wazalendo dhidi ya **Ndugu Mange Khamis Samwel** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Buseresere, Jimbo la Chato Kusini; na

ix. **Ndugu Saidi Hamisi Mikunya** mgombea udiwani kupitia Chama cha CUF, Kata ya Njinjo, Jimbo la Kilwa Kaskazini dhidi ya **Ndugu Juma Ahmadi Litembo** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Njinjo, Jimbo la Kilwa Kaskazini.

Hivyo, wagombea tajwa, wamerejeshwa katika orodha ya wagombea udiwani katika kata husika na waendelee na taratibu za kampeni za uchaguzi.

**5.0. Rufaa za udiwani zilizokataliwa:**

Zifuatazo ni rufaa kumi na saba (17) za wagombea udiwani zilizokataliwa: -

i. **Ndugu Rafii Kibwana Kombo** mgombea udiwani Kata ya Pangani Mashariki, Jimbo la Pangani kupitia Chama cha CHAUMMA dhidi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Kata ya Pangani Mashariki, Jimbo la Pangani;

ii. **Ndugu Chambale Ally Ally** mgombea udiwani Kata ya Namayuni, Jimbo la Kilwa Kaskazini kupitia Chama cha CUF dhidi ya **Ndugu Omary Ally Kipengele** mgombea udiwani kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Kata ya Namayuni, Jimbo la Kilwa Kaskazini;

iii. **Ndugu Abasi Kambi Legeza** mgombea udiwani Kata ya Visiga, Jimbo la Kibaha Mjini kupitia Chama cha ACT-Wazalendo dhidi ya **Ndugu Mohamedi Saidi Mpaki** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Visiga, Jimbo la Kibaha Mjini;

iv. **Ndugu Saini Joseph Peter** mgombea udiwani Kata ya Gwandi, Jimbo la Chemba kupitia Chama cha ACT-Wazalendo dhidi ya **Ndugu Dossa Ally Hassan** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Gwandi, Jimbo la Chemba;

v. **Ndugu Farida Mohamedi Kikoleka** mgombea udiwani Kata ya Miguruwe, Jimbo la Kilwa Kaskazini kupitia Chama cha Mapinduzi dhidi ya **Ndugu Halidi Mohamedi Kilete** mgombea udiwani kupitia Chama cha CUF Kata ya Miguruwe, Jimbo la Kilwa Kaskazini;

vi. **Ndugu Aron Machali Kulwa** mgombea udiwani Kata ya Bulungwa, Jimbo la Ushetu kupitia Chama cha ACT-Wazalendo dhidi ya **Ndugu**

**Kalwani Mteganoni Baluhya** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Bulungwa, Jimbo la Ushetu;

vii. **Ndugu Philbert Rugambwa Ngemera** mgombea udiwani Kata ya Kanyangereko, Jimbo la Bukoba Vijijini kupitia Chama cha CUF dhidi ya **Ndugu Hamimu Hassani Byeyombo** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Kanyangereko, Jimbo la Bukoba Vijijini;

viii. **Ndugu Sophia Ally Magimba** mgombea udiwani Kata ya Mzenga, Jimbo la Kisarawe kupitia Chama cha ACT-Wazalendo dhidi ya **Ndugu Mohammed Boniface Rubondo** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Mzenga, Jimbo la Kisarawe;

ix. **Ndugu Revocatus Christian Lukonge** mgombea udiwani Kata ya Kitangiri, Jimbo la Ilemela kupitia Chama cha Mapinduzi dhidi ya **Ndugu Donnard Ndaro Protas** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Kitangiri, Jimbo la Ilemela;

x. **Ndugu Thobias Joseph Mwamkonda** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Itope, Jimbo la Kyela dhidi ya **Ndugu Emily Edwin Mwasongwe** mgombea udiwani kupitia Chama cha ACT-Wazalendo Kata ya Itope, Jimbo la Kyela;

xi. **Ndugu Gunewe Godwin Marcel** mgombea udiwani Kata ya Kiseke, Jimbo la Ilemela kupitia Chama cha Mapinduzi dhidi ya **Ndugu Mwevi Ramadhani Mwevi** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Kiseke, Jimbo la Ilemela;

xii. **Ndugu Hawa Miraji Kihwele** mgombea udiwani Kata ya Igurusi, Jimbo la Mbarali kupitia Chama cha Mapinduzi dhidi ya **Ndugu Mussa Yusuph Ngupapa** mgombea udiwani kupitia Chama cha ACT-Wazalendo Kata ya Igurusi, Jimbo la Mbarali;

xiii. **Ndugu Majanjara Phares David** mgombea udiwani Kata ya Songambele, Jimbo la Kongwa kupitia Chama cha ACT-Wazalendo dhidi ya **Ndugu**

**Sadock Kajungu Peter** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Songambele, Jimbo la Kongwa;

xiv. **Ndugu Leah Meshack Masasi** mgombea udiwani Kata ya Majengo, Jimbo la Makambako kupitia Chama cha CHAUMMA dhidi ya **Ndugu Rosemary Lameck Lwiva** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Majengo, Jimbo la Makambako;

xv. **Ndugu Moses Marwa Mwera** mgombea udiwani Kata ya Muriba, Jimbo la Tarime Vijijini kupitia Chama cha ACT-Wazalendo dhidi ya **Ndugu Tumaini Mwita Chacha** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Muriba, Jimbo la Tarime Vijijini;

xvi. **Ndugu Zephania Godeni Chibaya** mgombea udiwani Kata ya Songambele, Jimbo la Kongwa kupitia Chama cha CHAUMMA dhidi ya **Ndugu Sadock Kajungu Peter** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Songambele, Jimbo la Kongwa; na

xvii. **Ndugu Nandonde Rashid Abdallah** mgombea udiwani Kata ya Mzinga, Jimbo la Kivule kupitia Chama cha CUF dhidi ya **Ndugu Job Isaack Ibrahim** mgombea udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi Kata ya Mzinga, Jimbo la Kivule.

Hivyo, kwa wagombea namba ***i*** ya kirumi hadi namba ***iv*** ya kirumi, ambao ni **Ndugu Rafii Kibwana Kombo** mgombea udiwani Kata ya Pangani Mashariki, **Ndugu Chambale Ally Ally** mgombea udiwani Kata ya Namayuni, **Ndugu Abasi Kambi Legeza** mgombea udiwani Kata ya Visiga na **Ndugu Saini Joseph Peter** mgombea udiwani Kata ya Gwandi, Tume imekubaliana na uamuzi wa wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi wa kata husika wa kutowateua kugombea nafasi ya udiwani.

Aidha, Tume imekubaliana na uamuzi wa wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi wa kata husika kwa warufaniwa namba ***v*** ya kirumi hadi namba ***xvii*** ya kirumi ambao ni **Ndugu Halidi Mohamedi Kilete** mgombea udiwani Kata ya

Miguruwe, **Ndugu Kalwani Mteganoni Baluhya** mgombea udiwani Kata ya Bulungwa, **Ndugu Hamimu Hassani Byeyombo** mgombea udiwani Kata ya Kanyangereko, **Ndugu Mohammed Boniface Rubondo** mgombea Kata ya Mzenga, **Ndugu Donnard Ndaro Protas** mgombea Kata ya Kitangiri, **Ndugu Emily Edwin Mwasongwe** mgombea Kata ya Itope, **Ndugu Mwevi Ramadhani Mwevi** mgombea Kata ya Kiseke, **Ndugu Mussa Yusuph Ngupapa** mgombea Kata ya Igurusi, **Ndugu Sadock Kajungu Peter** mgombea Kata ya Songambele, **Ndugu Rosemary Lameck Lwiva** mgombea Kata ya Majengo, **Ndugu Tumaini Mwita Chacha** mgombea Kata ya Muriba na **Ndugu Job Isaack Ibrahim** mgombea Kata ya Mzinga. Hivyo, waendelee na taratibu za kampeni za udiwani katika kata wanazogombea.

***"KURA YAKO HAKI YAKO JITOKEZE KUPIGA KURA"***

Imetolewa na:

Kailima, R. K

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**